BIBLIA KWA TASWIRA, AGANO LA KALE, KITABU CHA 22
2 SAMWELI

MUFALME WA MUNGU

(VISUALIZED BIBLE, Vol 22, OT, Godliness)
Mwandishi: Arlene S. Piepgrass
Muchapaji: Vernon Henkel
Imegeuzwa kwa Swahili Congo na watumishi wa Mungu katika DR Congo

© Bible Visuals International
PO Box 153, Akron, PA 17501-0153
Simu: 717-859-1131
www.biblevisuals.org

SOMO 1 - DAUDI ANAKUWA MUFALME WA ISRAELI

Kwa mwalimu kujifunza mbele: 2 Samweli sura 1 hadi 9

Shabaa ya somo: Kuonyesha kama Mungu yuko juu ya kiti chake cha ufalme mbinguni akitawala juu ya vitu vyote.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kwamba Mungu anasimika wafalme na watawala wa dunia (Angalia Danieli 4:25b)

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Waogope kwamba Mungu anayekuwa na uwezo wote, anachunguza kila jambo ndogo katika maisha yetu.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Waache Mungu awaongoze katika makusudio na mipango yao.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)

1. Heshima ya Daudi kwa Saulo na upendo kwa Yonatana (2 Samweli 1)
2. Yerusalema inageuka kuwa muji mukubwa wa Israeli (2 Samweli 5)
3. Ahadi ya Mungu (Agano) (2 Samweli 7)
4. Huruma ya mufalme (2 Samweli 9)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Tumainia Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe: katika njia zako zote umukiri yeye, naye ataongoza mapito yako.
Mezali 3:5-6

Maelezo kwa mwalimu:

Kuanza na Abrahamu (Mwanzo 12) mpaka wakati wa Samweli, Mungu ndiye alikuwa Mufalme wa Waisraeli. Kisha Waisraeli walitaka kuwa sawa na mataifa yaliyokuwa kandokando yao. Waliomba mufalme wa kidunia (1 Samweli 8). Kwa hiyo, Mungu akawapa yale waliyotaka. Akachagua Saulo kuwa mufalme wao. Kama Saulo angeliweza kumutii Mungu angeliweza kupata utawala wa ajabu. Kuliko vile, aliasi kwa makusudi. Na Mungu akamutupilia (1 Samweli 15:23-29).

Kwa nafasi ya Saulo, Mungu akachagua Daudi (1 Samweli 13:14). Ingawa vile, Saulo aliendelea kutawala Waisraeli kwa miaka mingi. Daudi alipigana na kushindia Saulo vita vingi. Halafu mufalme Saulo akapatwa na wivu juu ya Daudi na akatafuta kumwua. Kwa miaka mingi Daudi alipoteza wakati akimukimbia Saulo. Na kwa mara mbili Daudi angeweza kumwua. Lakini Daudi alikataa kugusa mufalme mupakaliwa wa Bwana. (1 Samweli 24 na 26). Alingojea Mungu amwondoe Saulo kwenye kiti na kumusimika yeye (Daudi).

Chunguza: Somo zinazopashwa kufundishwa zikifuata zile katika kitabu 21. Kwa kutumia vitabu vyote viwili, Historia ya Israeli na maisha ya Daudi vinaweza kueleweka.

Somo: Umekwisha kungojea kwa muda murefu zawadi uliyoahidiwa? (Acha wanafunzi washiriki ujuzi ule). Ulizani hautapokea zawadi ile? Haukukusudia kusema kama yule aliyetoa ahadi aliweza kusahau?

1. Heshima ya Daudi kwa Saulo na upendo kwa Yonatana (2 Samweli 1.)

Daudi aliambiwa na Mungu kwamba atakuwa mufalme wa Israeli atakayefuata. Daudi alikuwa anafanya nini wakati Samweli alienda kumupakaa mafuta kama vile mufalme? (Alikuwa akichunga kondoo, 1 Samweli 16:11). Ni nani aliyekuwa mufalme kwa wakati ule? (Saulo). Kwa nini Mungu alikuwa akitafuta mufalme mupya? (1 Samweli 13:14; 15:26). (Mwalimu: kwa kifupi urudilie matokeo yaliyomusukuma Mungu kumutupilia mufalme Saulo. (1 Samweli 13 & 15)

Saulo alipatwa na wivu juu ya Daudi na kumuchukia. Kwa muda wa miaka alitaka kumwua Daudi. Saulo alijua kama siku moja Daudi atamukomboa sawa mufalme.

Watu wengi walimupenda Daudi. Kweli, watu wengi walijiunga naye hata akawa na jeshi lake mwenyewe. Mara na mara Daudi na watu wake walipashwa kufichama mbali na mufalme Saulo. Wakati mwengine walijificha ndani ya mashimo (mapango). Kwa wakati mwengine walikimbilia Filistia. Wafilistini walikuwa majirani wao na maadui wao.

Daudi alingojea na kungojea kuwa mufalme. Lakini hakupoteza imani yake kwa Mungu. Aliamini Mungu atafanya yale aliyoahidi. Hata wakati Daudi alipata nafasi ya kumwua Saulo, alikataa kumugusa (1 Samweli 24:4-6; 26:8-10). Daudi alingojea Mungu amupe kiti cha ufalme.

Kungojea ni kugumu. Tunataka kujua ni kitu gani kitatokea. Tunataka kitokee kwa haraka. Mungu anatuambia kama iko "anatimiza yale aliyopanga kwa ajili yetu." (Yobu 23:14). Anatumika maneno yote pamoja kwa ajili ya mema. Lakini hayuko haraka.

(Mwalimu: Acha wanafunzi wasome kwa sauti kubwa aya zimoja kati ya hizi: Zaburi 27:14; 37:7; 40:1; 46:10; 62:1, 5, 8; Isaya 30:18; 40:31)

Wakati unakosa uvumilivu na kutaka mambo yatendeke kwa haraka, kumbuka Daudi. Mungu hawezi kusahau ahadi yake. Naye hawezi kukusahau.

Daudi akatimiza miaka 30 (2 Samweli 5:4). Yeye pamoja na watu wake walikuwa katika muji wa Ziklagi. Siku moja, mutu moja toka katika jeshi la Saulo alikuja katika muji akikimbia. Nguo zake zilikuwa zimepasuka. Alikuwa na vumbi juu ya kichwa chake. Hizi zilikuwa alama za kutambulisha kama mutu amekufa. Yule askari akaanguka kwenye miguu ya Daudi. Daudi akauliza: "Unatokea wapi? Kulitokea nini?"

Onyesha taswira 1: Yule mutu akajibu: "Ninatokea katika jeshi la Saulo. Tumeshindwa na Wafilistini. Maelfu ya waaskari wameuawa. Mufalme Saulo na mwana wake Yonatana wamekufa vilevile. Taji la mufalme ndilo hili na kikomo chake kimoja."

Unafikiri Daudi alifurahi wakati alisikia habari hii? (Acha wanafunzi watoe mawazo). Sasa nani ndiye atakayekuwa mufalme? (Daudi). Katika siku zile kila mufalme mupya aliweza kuua jamaa lote la mufalme aliyetangulia. Unafikiri Daudi alifanya vile?

Hapana! Daudi hakuamuru waue jamaa lote la Saulo. Wala hakupaza sauti kwa furaha. Pahali pake, yeye pamoja na watu wake wote walipatwa na uchungu. Kwa huzuni walipasua nguo zao kwa kuonyesha sikitiko na maumivu yao. Walilia siku nzima kwa ajili ya Saulo na Yonatana.

Kwa nini kifo cha Yonatana kilimuhuzunisha Daudi? (Kumbusha urafiki wa Daudi na Yonatana, 1 Samweli 18 na 20). Daudi hataona tena katika dunia rafiki yake mwema.

Kwa nini Daudi aliomboleza sababu ya Saulo? Yule aliyetaka kumwua? (Daudi alimuheshimu Saulo kama vile mufalme aliyechaguliwa na Mungu kwa kutawala Israeli. Kwa sababu Daudi alimupenda Mungu, alumuhurumia Saulo). Daudi aliandika wimbo muzuri sana kwa ukubusho wa Saulo na Yonatana. (Soma 2 Samweli 1:24-27)

2. Yerusalema inageuka kuwa muji mukubwa wa Israeli (2 Samweli 5.)

Sasa Daudi amekuwa mutu mukubwa sana katika Israeli. Ni nani amemupa madaraka hayo? (Mungu). Ataweza kusahau Mungu kama vile Saulo alivyofanya?

Mungu alisema nini juu ya Daudi? (Mutu anayependeza moyo wake mwenyewe, 1 Samweli 13:14). Daudi alitaka kumupendeza Mungu zaidi kuliko kitu kingine chochote katika dunia.

Palepale Daudi aliomba Mungu. Akaomba hivi: "Ninaweza kutoka Ziklagi na kwenda katika muji moja wa miji ya Yuda?" (Angalia 2 Samweli 2:1) BWANA akajibu: "Ndiyo, Daudi wende katika Yuda." Daudi akauliza: "Niende wapi?" BWANA alisema: "Wende katika muji wa Hebroni." (Mwalimu: Rudilia tena Mezali 3:5-6. Utumie kwa wanafunzi.)

Daudi, jamaa lake, na wafuasi wake wote kwa utiifu walikwenda Hebroni. Kule, watu wa Yuda wakamupakaa mafuta kuwa mufalme.

Lakini sio Waisraeli wote waliokubali Daudi kama mufalme. Wamoja walijaribu kumufanya Isiboseti, mwana wa Saulo kuwa mufalme. Je, waliweza? (Hapana) Kwa nini? (Kwa sababu Mungu alitupilia mbali jamaa la saulo. Kwa pahali pake alichagua Daudi, 1 Samweli 15:28).

Kwa muda wa miaka saba, Daudi alitawala jimbo la Yuda akiwa Hebroni. Alipashwa kungojea wakati wa Mungu kwa kutawala juu ya Waisraeli wote.

Siku moja habari ikasambaa katika inchi kama Isiboseti amekufa. Viongozi wote wa Israeli walimwendea Daudi kule Hebroni. Walitia mukazo: "Tunataka wewe kuwa mufalme wetu. Saulo alipokuwa mufalme, uliongoza majeshi yetu. Uko ndugu yetu. Bwana alisema utakuwa kiongozi wetu."

Kwa mwisho, Daudi akavalishwa taji kuwa mufalme wa Waisraeli wote. Ahadi ya Mungu kwa Daudi ikatimilika! Ulikuwa wakati muzuri namna gani huo! Watu wote walisherekea kwa siku tatu! (Angalia 1 Mambo ya siku 12:23, 29, 40)

Kama vile mufalme, Daudi alisimamia mambo ya lazima. Kwanza, Daudi alishinda maadui ndani na kandokando ya Yerusalema. Kisha akaondoka Hebroni kwenda Yerusalema. Akaita Yerusalema "Muji wa Daudi." Na akaufanya muji mukubwa wa Israeli.

Onyesha taswira 2: Nyuma ya hayo, mufalme Daudi alileta sanduku la Mungu Yerusalema. Sanduku lilipashwa kulindwa katika Pahali Patakatifu ndani ya Hema ya kusanyiko. (Kumbusha wanafunzi kama Waisraeli walimuabudu Mungu ndani ya Hema ya kusanyiko. Mungu alifanya uwepo wake uonekane juu ya sanduku katika Pahali Patakatifu sana.)

Acha nikuelezee kitu kilichotokea miaka mingi mbele ya haya. Waaskari wamoja waliomwasi Mungu, walitwaa sanduku la Mungu wakati wa vita. (Angalia 1 Samweli 4). Wafilistini wakaleta sanduku na kulipeleka katika inchi yao. Kwa sababu ya hiyo, Mungu akaleta hukumu kwa Wafilistini kwa muda wa miezi saba. Akawaazibu kwa majipu na panya wa kila aina. Kwa mwisho, Wafilistini wakarudisha sanduku kule Israeli. Kwa miaka 20, lililindwa katika nyumba ya Mwisraeli moja. Sasa, mufalme Daudi akaweka sanduku ndani ya Hema ya kusanyiko. Pale ndipo nafasi yake. Daudi alifanya Yerusalema kuwa nafasi kubwa ya kuabudia kwa Waisraeli. (Linganisha na Kumbukumbu 12:5)

Vilevile mufalme Daudi alijenga nyumba nzuri ya kifalme (2 Samweli :11). Alikuwa anaishi ndani ya mashimo na kutangatanga kwa miaka. Sasa kwa mwisho Daudi alitulia.

3. Ahadi ya Mungu (agano) (2 Samweli 7.)

Daudi alichagua watu waaminifu, wanaomupenda Mungu kuwa washauri wake (Zaburi 101:6). Mumoja kati ya watu wale alikuwa ni Natana. Alikuwa nabii wa Mungu na rafiki mwema wa mufalme Daudi.

Siku moja Daudi akasema: "Natana, ninaishi katika nyumba kubwa. Lakini sanduku la Mungu liko katika hema. Ningependa kujenga hekalu nzuri kabisa kwa ajili ya Bwana."

Natana akajibu: "fanya vile unavyotaka. Bwana yuko pamoja nawe." Unafikiri tamaa ya Daudi ilikuwa nzuri? (Acha wanafunzi wajibu)

Kwa usiku ule ule, Mungu akasema na nabii. Bwana alisema: "Natana, toa ujumbe huu kwa Daudi. Hapashwi kunijengea hekalu nzuri. Ni vizuri kwamba anataka kufanya kitu kwa ajili yangu. Kuliko vile nitafanya kitu kikubwa zaidi kwa ajili yake.

Bwana alisema zaidi na Natana. Na Natana alipeleka ujumbe wa Mungu kwa mufalme Daudi.

Onyesha taswira 3: Natana akaanza: "Ulikuwa kijana wakati Mungu alikuchagua kwa kuongoza watu wake. Bwana alikupatia wewe na jeshi lako ushindi juu ya maadui wako. Alifanya jina lako kuwa kubwa. Mungu anasema atalifanya kubwa zaidi. Atapatia Waisraeli inchi itakayokuwa yao kwa milele. Utakapokufa, mwana wako ndiye atakayejenga hekalu kwa ajili ya Mungu. Na atatawala watu wa Mungu. Akimwasi Mungu, Mungu atamuazibu. Lakini Mungu hatamuondoa kwa kiti cha kifalme. Daudi, uzao wako wa kifalme utadumu kwa milele."

Ahadi hii ya nyuma ilitimilika miaka mamia baadaye. Bwana Yesu Kristo alizaliwa katika jamaa la wazao wa Daudi (Matayo 1:1). Atakaporudia duniani, atakaa juu ya kiti cha kifalme cha Daudi (Luka 1:32-33). Halafu Bwana Yesu Kristo atatawala dunia (Ufunuo 11:15). Hakuna anayejua wakati haya yatakuwa.

Miaka mingi mbele Daudi aishi, Mungu aliahidi kutuma yule atakayeshinda Shetani. (Mwanzo 3:15). Alirudilia upya ahadi hii kwa Daudi. Alieleza kwamba Mutu huyu atatokea katika jamaa la Daudi.

Daudi alisikiliza ujumbe wa Mungu. Halafu akaingia ndani ya hema na kukaa mbele ya Bwana. Daudi akaabudu Mungu na kumusifu kwa ajili ya ahadi zake za ajabu. Daudi akaomba hivi: "Bwana, mimi ni nani hata umenipatia upendeleo kama huu? Mimi si wa lazima. Jamaa langu si la lazima. Ni mema ya namna gani umenitendea! Ee Bwana Mungu, Wewe ni Mukubwa namna gani! Hakuna anayekuwa kama Wewe. Hakuna Mungu mwengine zaidi yako. Acha jina lako litukuzwe kwa milele!"

4. Huruma ya mufalme (2 Samweli 9.)

Mara na mara, mufalme Daudi alifikiri juu ya rafiki yake Yonatana ambaye sasa amekufa. Daudi alikumbuka: Nimeahidi nitakuwa mwema kwa jamaa lake. Akauliza watumishi wake: "hakuna mutoto yeyote wa Yonatana anayekuwa muzima?"

Wakajibu: "Ndiyo, Yonatana, mwana wa mufalme iko na mwana anayeitwa Mefiboseti. Angali muzima. Saulo alipouawa, mulezi wake akakimbia naye. Katika haraka yake, mulezi yule akamwangusha. Akakuwa kiwete - kilema wa miguu yote mbili - hata sasa."

Daudi akaamuru: "Mumutafute sasa hivi." Mefiboseti alipokea amri ya mufalme, akaangaika. Alifikiri, tate yangu, mufalme Saulo, alimuchukia Daudi. Alitaka kumwua Daudi. Sasa mufalme Daudi ataniua kwa kulipiza kisasi. Kila mara wafalme wanaua jamaa za maadui zao.

Mefiboseti aliogopa alipoonyeshwa kwa mufalme Daudi. Akaanguka uso wake mpaka chini kwa kuheshimu mufalme.

Onyesha taswira 4: Daudi akazungumuza kwa upole na Mefiboseti. Mufalme akasema: "usiogope, sitakuzuru. Nilimupenda sana baba yako Yonatana. Kwa sababu yake, ninataka kukutendea mema. Nitakurudishia mashamba yote yaliyokuwa ya tate yako. Ziba, mutumishi wa zamani wa tate yako pamoja na wana wake, watakulimia mashamba yale. Lakini utaishi pamoja nami katika nyumba ya kifalme. Utakula pamoja nami mezani."

Mefiboseti akalia: "Ee mufalme Daudi! Kwa nini unanitendea mema mimi ninayekuwa kama imbwa iliyokufa?"

Mefiboseti hakufanya kitu kwa kustahili wema toka kwa mufalme. Aliheshimishwa sababu alikuwa mwana wa Yonatana.

Wema wa Daudi ni picha nzuri ya upendo wa Mungu kwa ajili yetu. Mungu alitutafuta. Sisi hatufai. Hatustahili upendo wake. Lakini kwa ajili ya Kristo, Mungu anasamehe wale wanaoamini Mwana wake. (Waefeso 4:32).

Mefiboseti alikubali toleo la Daudi. Akahamia kwenye nyumba ya kifalme kule Yerusalema. Alikula na kushiba kwenye meza ya mufalme.

Leo, Mungu - Mufalme juu ya wafalme - anatutolea wokovu. Anataka kutuokoa toka zambi kwa njia ya Mwana wake, Kristo Yesu, aliyekufa kwa ajili yetu. Lakini tunapashwa kukubali toleo lake. Tuseme Mefiboseti alikataa toleo la mufalme. Angeliweza basi kufurahia baraka ya maisha ya ndani ya nyumba ya mufalme? (Hapana).

Unaweza kukataa kumukubali Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wako. Kwa kumukataa Mwana wa Mungu, utatengwa mbali naye kwa milele. Na utahukumiwa kwa siku zote. Halafu, kwa siku hii ya leo, amini Yesu kama vile Mwokozi wako.

SOMO 2 – ZAMBI ZA MUFALME DAUDI

Kwa mwalimu kujifunza mbele: 2 Samweli sura 10 hadi 12

Shabaa ya somo: Kuonyesha kama Daudi ni mutu ambaye alipendwa sana na Mungu, hakuwa mukamilifu.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kwamba Mungu anaazibu zambi lakini anasamehe mwenye zambi anayekiri zambi zake.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Kuwa na uhakika wa zambi katika maisha yao.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kukiri zambi zote wanazojua; kukubali musamaha wa Mungu; kutafuta kusihi katika utiifu wa Neno la Mungu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Wanawake wengi wa Daudi (2 Samweli 5:13)
2. Daudi na Batiseba (2 Samweli 11:1-5)
3. Daudi na Uria (2 Samweli 11:6-27)
4. Daudi na Natana. (2 Samweli 12:1-23)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Tumainia Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe: katika njia zako zote umukiri yeye, naye ataongoza mapito yako."
Mezali 3:5-6

Maelezo kwa mwalimu:

Fikiri juu ya haya**:** Kwa miaka 20, Daudi alitawala Israeli vizuri. Aliishi kwa ushirika na Mungu. Mungu alimupatia ushindi juu ya maadui wake. Waisraeli walisitawi. Watu walimupenda Daudi. Daudi akakuwa mumoja wa viongozi wakubwa wa kiroho wa Agano la Kale.

Mufalme Daudi alikuwa na nguvu na kufanikiwa. Labda hii ndiyo sababu alianza kuasi Mungu. Daudi hakuwa mukamilifu.. hakutenda kila mara sawa na "mutu anayetia moyo wake nyuma ya Mungu." Lakini Daudi alikiri zambi zake na Mungu akamusamehe. Ingawa hivyo, Daudi alipata mateso ya azabu kwa ajili ya zambi zake. Hii ilileta taabu nyingi katika maisha yake, jamaa lake, na taifa lake.

Somo: Unaweza kukumbuka wakati moja ulikosa kutii kwa kusudi wazazi wako? Ulijisikia namna gani? Ulikuwa na furaha? Wazazi wako walifurahi walipotambua kutokutii kwako? Waliweza kukuazibu? Kwa nini? Waliendelea kukupenda? Uliweza kusema wakuhurumie? Waliweza kukusamehe?

Leo tutajifunza moja kati ya mambo ya kuhuzunisha katika Biblia. Ni somo juu ya zambi. Na kila mara zambi inaleta taabu. Daudi alielezwa kuwa nani katika Biblia? (Moyo wale ulipendeza Mungu). Hii ina maana ya kusema kama alikuwa mukamilifu? (Hapana). Maana yake Daudi alimupenda Mungu kwa moyo wake wote. alitaka kwa kweli kumupendeza Mungu.

Daudi alikuwa mufalme muzuri, aliyechaguliwa na Mungu. alitawala Waisraeli kwa miaka 20. Watu wote walimupenda. Bwana alimusaidia Daudi kuwashinda maadui wake waliokuwa kandokando ya Israeli. Kwa hiyo, yale mataifa yaliyopakana naye yalimuogopa.

1. Wanawake wengi wa Daudi (2 Samweli 5:13.)

Kwa wakati mwingi, mufalme Daudi aliomba Mungu amwongoze. Kwa wakati mwingine alimutii Mungu. lakini kwa jambo moja Daudi alimwasi Mungu. Alikuwa na wanawake wengi.

Mungu alimupa Adamu wanawake wangapi? (moja). Nyuma Mungu akaleta sheria inayosema wafalme hawapashwi kuwa na wanawake wengi. (Soma kwa sauti Kumbukumbu 17:14-17). Mufalme Daudi alizarau sheria hii.

Onyesha taswira 5: Wakati Daudi alihama toka Hebroni kwenda Yerusalema, akatwaa wanawake wengi. Hakumwuliza Mungu juu ya hayo. Kuliko vile alitenda sawa na wafalme wapagani waliokuwa kandokando ya Israeli.

2. Daudi na Batiseba (2 Samweli 11:1-5.)

Ilikuwa wakati wa mwanzo wa mwaka mupya. Waaskari wa Daudi walikuwa inje ya muji wakipigana na maadui wa Israeli. Mufalme Daudi hakutoka kwenda kwa vita pamoja na jeshi lake. Akatuma Jemadari Yoabu kuongoza.

Siku moja mangaribi Daudi alikuwa akizunguuka zunguuka juu ya dari la bustani. Akaangalia chini, akaona mwanamuke mwenye sura nzuri sana akioga.

Onyesha taswira 6: Daudi akaita mutumishi wake moja. Akaamuru hivi: "Kwenda kuangalia yule mwanamuke mwenye kupendeza sana ni nani!"

Nyuma kidogo yule mutumishi akaleta habari. Akasema: "Mufalme Daudi, yule bibi ni Batiseba. Mume wake ni Uria, mumoja wa waaskari wako. Yuko katika jeshi lake akipigana chini ya uongozi wa Jemadari Yoabu."

Daudi akaamuru: "Umulete Batiseba kwenye nyumba yangu!" Unafikiri Daudi aliomba Mungu kwa ajili ya hayo? (Hapana). Ikiwa aliomba, Bwana angeweza kumwambia nini? (Acha wanafunzi wajibu. Tia mukazo kwamba hii ilikuwa zambi.)

Sheria ya Mungu inaamuru kama hakuna mutu atakayetwaa muke wa mutu mwengine (Kutoka 20:14). Lakini mufalme Daudi hakufikiri juu ya Bwana. Alikuwa anafikiri tu juu yake mwenyewe. Alitaka njia yake mwenyewe. Hakufurahi bila kuwa na Batiseba. Kwa hiyo, mutumishi wa Daudi akaleta Batiseba katika nyumba.

Kesho yake asubui, Batiseba akarudia kwake. Maisha katika nyumba ya kifalme yaliendelea kama kawaida. Daudi alitumaini yule mutumishi hatasema juu yake.

Lakini mutu moja hakuhitaji kuambiwa. Bwana Mungu aliona yale mufalme Daudi aliyofanya. Neno la Mungu linasema: "Mujue ya kuwa zambi yenu itawapata." (Hesabu 32:33)

Nyuma ya majuma Daudi akapokea ujumbe toka kwa Batiseba. Unasomeka hivi: "Mufalme Daudi, nitapata mutoto - mutoto wako."

Daudi akafikiri, nitafanya nini? Watu wasisubutu kujua yaliyotendeka. Uria hapashwi kupata habari juu ya hayo. Daudi alikuwa akijaribu kupata njia ya kuficha zambi yake. Kwa mwanzo, mufalme Daudi alikuwa anauliza Mungu apate kumwonyesha la kufanya. Kwa nini hakumwuliza Mungu kwa wakati huu? (Daudi alitambua kwamba alifanya zambi. Alijua kama hakumupendeza Mungu.)

3. Daudi na Uria (2 Samweli 11:6-27.)

Daudi akajifunza mupango. Akatuma mbio ujumbe kwa Jemadari Yoabu: "Umutume sasa hivi askari wako Uria kwa nyumba ya kifalme."

Onyesha taswira 7: Uria alipofika, mufalme alitenda kama vile mambo yote yalikuwa mazuri. Akauliza: "Mambo yanaendeka namna gani katika vita?"

Uria alifasiria: "Vita inaendeka vizuri." Daudi akajibu: "Hii ni habari njema. Uria, sasa ninataka wende kwako. Upitishe usiku pale. Unahitaji kupumzika sababu ya kupigana."

Daudi alitumaini kufunika zambi yake. Ingawa hivyo, Uria alibaki kwenye mulango wa nyumba ya kifalme usiku wote.

Mufalme Daudi akapata habari ile asubui. Akauliza: "Uria, kuna jambo gani? Kwa nini haukwenda kwako kwa muke wako usiku uliopita? Ulikuwa mbali kwa vita kwa muda murefu."

"Mufalme Daudi, singeliweza kwenda kwangu. Nimefikiri juu ya waaskari wetu wote na Jemadari Yoabu wanaolala inje. Kwa nini niende kupumzika nyumbani wakati wako wanatupigania?"

Mufalme angeliweza kukiri zambi yake kwa Bwana. Kuliko vile, alikuwa na wazo lingine. Akamwandikia Jemadari Yoabu barua na kuitia muhuri. Kesho yake asubui, akamwambia Uria: "Rudia kwa kazi yako. Na tafazali umupatie Jemadari Yoabu barua hii."

Wakati Yoabu alivunja muhuri wa barua ya mufalme, akasoma: “Tia Uria kwa mustari wa mbele wa vita. Uwe hakika kama atauawa!”

Fikiri juu ya haya! Mufalme Daudi alifanya shauri mbaya la kumuuwa Uria. Alijua sheria ya Mungu (Kutoka 20:13). Lakini aliizarau. Alimwasi Mungu kwa kusudi.

Nyuma, mujumbe akafika kwa nyumba ya mufalme akiwa na habari toka kwa Jemadari Yoabu. “Tulisogelea kuta za muji. Waaskari wao wenye nguvu sana wakatoka kutupiganisha. Waaskari wetu - wengi - pamoja na Uria - waliuawa.”

Daudi alifikiri, ni faraja ya namna gani hii! Sasa ninaweza kumuleta Batiseba kwa nyumba yangu kama vile muke wangu. Mambo yote yatakuwa sawa.

Je mambo yote yalikuwa mazuri? Nani aliyeona yote yaliyotendeka? (Bwana Mungu.) Sikiliza yale Biblia inayosema. (Soma polepole 2 Samweli 11:27 - ukitia mukazo juu ya maneno ya mwisho.)

4. Daudi na Natani (2 Samweli 12:1-23.)

Miezi mingi ilipita. Halafu siku moja mufalme Daudi pamoja na Waisraeli wote wakafurahi. Mutoto mwanaume alikuwa amezaliwa katika nyumba ya kifalme.

Lakini Mungu hakupendezwa. Alihuzunika. Mutumishi wake, Daudi amefanya zambi. Kwanza mufalme Daudi alikuwa amemuvuta Batiseba kwenye nyumba ya kifalme. Tena alifanya mupango kusudi mume wake Uria auawe.

Unafikiri Daudi alifurahi kwa kweli? Hapana. Alijua kama amefanya makosa. Alitambua kwamba ametendea wengine bila haki. Alijua kwamba alimwasi Mungu. alijaribu kusahau haya yote. Lakini hakuweza. (Soma Zaburi 32:3-4). Hakuna mutu anayezuru wengine na kuwa na furaha.

Kwa nini Mungu hakumukataza Daudi kualika Batisea katika nyumba ya kifalme? Hatujui. Lakini Mungu alitupatia uhuru wa kuchagua. (Soma Yoshua 24:15). Anataka sana tumutii yeye sababu tunapashwa.

Mara kwa mara utashawishiwa kufanya zambi. Bwana atakusaidia usishindwe na kishawishi. (Angalia 1 Wakorinto 10:13). Lakini mufalme Daudi hakujali Mungu. Alitaka Batiseba. Ingawa hivyo, Mungu alimujali Daudi. Siku moja, akatuma Natana, nabii wake kwenye nyumba ya mufalme.

Natana akaanza hivi: “Mufalme Daudi, kitu kibaya kimoja kilitendeka katika ufalme wako.” Daudi akasema kwa bidii: “Uniambie juu ya lile.”

Natana akasema: “Sikiliza vizuri. Kulikuwa watu wawili katika muji. Mumoja alikuwa tajiri na alikuwa na kondoo na wana kondoo wengi sana. Yule mwengine alikuwa masikini. Alikuwa tu na mwana-kondoo mudogo. Yule mwana-kondoo akakuwa munyama rafiki wa watoto wake. Yule mwana-kondoo alikunywea kwa kopo moja na yule mutu masikini na alikulia kwa sahani moja naye. Angalia jinsi jamaa lilivyopenda yule mwana-kondoo mudogo!”

Natana akaendelea kusema: “Siku moja yule tajiri akapata mugeni. Yule tajiri alitaka kutayarishia mugeni wake chakula kizuri sana. Akakusudia kutouwa hata mumoja wa wana-kondoo wake kwa ajili ya karamu. Pahali pake akatwaa yule mwana-kondoo moja tu wa yule masikini. Akamwua, akamuchoma na kumupatia mugeni wake!”

Mufalme Daudi akapatwa na hasira alivyokuwa akisikiliza. Akasema kwa sauti kubwa: “Mutu yule anapashwa kuuawa! Anapashwa kumupa yule masikini wana-kondoo wane kwa ajili ya yule moja aliyeiba!”

Natana akamwangalia Daudi ndani ya macho. Kwa heshima akasema: “Mufalme Daudi, wewe ndiwe yule tajiri!”

Daudi alifazaika. Natana aliendelea kusema: “Sikiliza yale Bwana Mungu wa Israeli aliyosema juu yako.” (Mwalimu: Soma polepole kwa sauti kubwa 2 Samweli 12:7-9).

Mungu alimukumbusha Daudi yote aliyofanya kwa ajili yake. Kisha Bwana akasema: Umezarau sheria zangu. Umetenda kwa uovu. Kwa hiyo, wewe na jamaa lako mutaazibiwa. Daudi umetenda kwa siri. Lakini nitakuazibu wazi wazi.”

Daudi akamwambia Natana hivi: “Nimemukosea Bwana!” Mufalme Daudi alihuzunika sana. Mungu aliona moyo wa mufalme na kutambua kama alikuwa mwenye ukweli.

Natana akajibu: “Ndiyo, Daudi, umemukosea Mungu. lakini anakuhurumia. Hautakufa kwa ajili ya zambi zako sawa vile ulivyostahili. (Angalia Walawi 20:10). Umeleta haya kubwa kwa jina la Bwana. Umemupa adui zake sababu ya kumutukana. Kwa sababu ya hii, mutoto wako aliyezaliwa na Batiseba atakufa!”

Halafu Natana akaondoka. Na palepale Daudi akapata habari kwamba mwana wake ni mugonjwa sana.

Onyesha taswira 8: Akianguka chini, Daudi akaomba. “Ee Bwana Mungu, tafazali usiache mutoto wangu akufe.” Na kwa muda wa siku saba muchana na usiku, Daudi alikataa kula. Aliendelea kuomba Mungu amwokoe mwana wake. Lakini kwa siku ya saba, mutoto akakufa.

Daudi alikuwa na moyo wenye kuvunjika sababu alimwasi Mungu. Sasa alitwaa muda wa kufikiri. Na akaomba - Yoo, aliomba namna gani! (Wanafunzi wasome polepole sehemu za maombi ya Daudi katika Zaburi 51:1-3, 7, 10, 12, 16).

Daudi alikuwa akiomba: “Mungu mupendwa, unihurumie. Nimekukosea sana. Una haki ya kuniazibu ginsi unavyotaka. Ninastahili ile. Unataka niwe mwaminifu na wa haki. Nimekuwa mwenye zambi. Unisafishe na nitakuwa mweupe kama teluji. Uniumbie moyo safi, ee Mungu. Weka ndani yangu roho ya haki. Unirudishie furaha kamilifu tena. Ninaweza kwenda kwa Hema ya kusanyiko na kutoa sadaka kwa ajili ya zambi zangu. Lakini haya siyo yale unayotamani. Unataka nisikitike kwa kweli na yale niliyotenda. Ninatubu, Bwana mupendwa. Tafazali unisamehe. Halafu nitawaambia wengine juu ya musamaha wako. Nitaimba utukufu wako kwa watu wote!”

Kwa nini Bwana aliweza kumusamehe mufalme?

1. Daudi alikubali zambi zake.
2. Daudi alisikitika kwa kweli kwa ajili ya zambi zake.
3. Daudi aliomba Mungu amusamehe.

Bwana Mungu aliendelea kumupenda Daudi na alimusamehe. Lakini alimwazibu. Ni mara ngapi tunakuwa kama Daudi! Tunachagua kutenda mabaya. Mungu anasema: “yeye anayefunika makosa yake hatasitawi: lakini yeye anayekiri na kuyaacha atapata rehema.” (Mezali 28:13).

Daudi alikuwa mwenye zambi. Ijapokuwa alimupenda Mungu sana, hakuwa mukamilifu. Mungu ameandika zambi ya Daudi ndani ya Biblia kwa kutufundisha somo fulani. Acha tuandike maneno ya kweli tuliyojifunza:

1. Kutojaribiwa kufanya zambi: Palepale tunapashwa kumwita Bwana kwa kutusaidia kusema “Hapana” (Angalia Yakobo 4:7-8)
2. Usijaribu kuficha zambi. Uikiri na kuomba Mungu akusamehe (1 Yoane 1:9)
3. Mungu anatuona wakati wote (Yobu 34:21)
4. Mungu anachukia zambi (Waroma 6:23a)
5. Mungu anapenda watoto wake, lakini anawaazibu wakati wanafanya zambi (Waebrania 12:6).

Mungu anasema sisi wote tuko wenye zambi (Waroma 3:23; 3:10). Wote tunastahili azabu ya milele. Alituma Mwana wake, Yesu kufa kwa ajili ya zambi zetu. Bwana Yesu alifufuka toka ndani ya kaburi. Anakutolea uzima wa milele pamoja naye mbinguni (Yoane 11:25-26). Unaweza kupata uzima ule kwa kumupokea Kristo kama Mwokozi wako. Unaweza kufanya vile sasa hizi?

SOMO 3 - MUFALME DAUDI ANATESWA KWA AJILI YA ZAMBI ZAKE.

Kwa mwalimu kujifunza mbele: 2 Samweli 13 hadi 18

Shabaa ya somo: Kuonyesha kwamba Mungu anaadibisha watoto wake wanaofanya zambi kwa kusudi.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kwamba anavuna kile anachopanda.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Kuwa na tamaa ya kuepuka zambi.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kuomba kwa bidii kusudi wasipate kushindwa na majaribu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Uasherati wa Amunoni. (2 Samweli 13:1-17)
2. Ukali wa Abusaloma (2 Samweli 13:18-39)
3. Uasi wa Abusaloma (2 Samweli 14:1-18:33).
4. Toba ya Daudi (2 Samweli 19:1-8)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Tumainia Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe: katika njia zako zote umukiri yeye, naye ataongoza mapito yako.
Mezali 3:5-6

Maelezo kwa mwalimu:

Kumbuka haya: Ahadi ya Mungu ni hii: "Tukikiri zambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote. (1 Yoane 1:9). Bwana anaonya: "Musidanganywe, Mungu hazihakiwi, yoyote mutu anayopanda, ndiyo atakayovuna." (Wagalatia 6:7)

Mungu ni Baba mwenye kupenda sana anayeadibisha watoto wake wanaotenda zambi. (Angalia Waebrania 12:5-8). Palepale Bwana alimusamehe Daudi wakati alikiri zambi zake (2 Samweli 12:13). Lakini matendo mabaya ya Daudi yalisikitisha jamaa lake na taifa lake. Yeyote anayefanya zambi analeta taabu kwa maisha ya wengine.

Daudi alijua vizuri azabu ya Baba wa mbinguni mwenye upendo. Hakupata hukumu ya Mungu Mutakatifu. (Waebrania 12:6)

Somo: Umekwisha kupanda mbegu za maua ao za mboga? (Acha wanafunzi waseme yale wamekwisha kupanda.) Wakati unapanda punje za mihindi, nini inaota? (muhindi). Je unavuna mahalagi toka kwenye muti wa muhindi? (Hapana, unavuna kile ulichopanda).

Aya moja ndani ya Biblia inasema: "Musidanganywe; Mungu hazihakiwi: yoyote mutu anayopanda, ndiyo atakayovuna." (Wagalatia 6:7). Aya hii haisemi juu ya mbegu zilizopandwa. Inasema juu ya mambo tunayofanya kila siku. Kama tunatenda mabaya kila wakati, tutachukua matokeo yake. Kwa kuasi kwa makusudi wale wanaokuwa na madaraka juu yako, utapata taabu. Hii ndio matokeo ya uasi wako. Wazazi wazuri wanawaadibisha watoto wao sababu wanawapenda. Wanataka kuwasaidia wapate kujua yanayokuwa mazuri na mabaya.

Mungu anatupenda. Anataka tumutii Yeye. Utii kwa Bwana unatuletea furaha na raha. Mungu alimupenda Daudi na mufalme Daudi alimupenda Mungu. Lakini Daudi alifanya nini iliyomuchukiza Bwana? (Alitwaa mwanamuke wa mume mwengine na kafanya mupango kusudi mume wake auawe). Je, Mungu alimusamehe Daudi? (Ndiyo) Daudi aliendelea kuwa mufalme. Alikuwa amechaguliwa na Mungu. Lakini Natana alimutolea maonyo. "Daudi, zambi yako itakuletea taabu wewe na jamaa yako." Taabu hiyo itakuwa matokeo ya zambi ya Daudi.

1. Uasherati wa Amunoni (2 Samweli 13:1-17.)

Unakumbuka kama mufalme Daudi alikuwa na wanawake wengi? Kulikuwa ubaya wowote kwa ile? (mupango wa Mungu ulikuwa mume na muke kuwa mumoja, Mwanzo 2:24)

Mumoja kati ya wanawake wa Daudi alikuwa na mwana aliyeitwa Amunoni (2 Samweli 3:2). Pamoja na muke mwengine, Daudi alipata binti aliyeitwa Tamari. Tamari alikuwa kijana binti mwenye sura nzuri sana. Amunoni akamupenda. Alitaka kulala naye bila kuwa wenye kuowana. Lakini hii imekatazwa na Mungu. Kwa sababu ni zambi. Kila siku Amunoni alikuwa akimuangalia Tamari. Kila siku alikuwa mwenye huzuni sababu hakuweza kumupata. Amunoni akakuwa mwenye moyo wenye kuvunjika kupita kiasi. Rafiki yake Yonadabu alihusika naye.

Onyesha taswira 9: Yonadabu akauliza: "Ni nini isiyoendeka kwako? Unahuzunika kila mara. Uniambie nini inayokuhuzunisha."

Amunoni akamujibu: "Ninamupenda dada yangu Tamari." Yonadabu akasema kwa kushangaa: "Mwana wa mufalme anapashwa kupata chochote anachotaka! Acha nikuambie cha kufanya. Ujifanye mugonjwa. Umwombe baba yako, mufalme Daudi atume dada yako Tamari katika chumba chako akutayarishie chakula. Umwambie kama utapona Tamari akifanya vile."

Amunoni alipenda wazo la Yonadabu. Halafu ikakuwa wakati Tamari alitayarisha chakula kizuri kwa ajili ya Amunoni. Kuliko kula, Amunoni akamukaza Tamari alale naye.

Daudi aliposikia yale Amunoni alifanya, akakasirika sana. Alijua Neno la Mungu. (Angalia Walawi 20:17). Lakini hakumwazibu Amunoni.

Yonadabu alikuwa kwa kweli rafiki muzuri? (Muwe na muda wa kuzungumuza. Tia mukazo: Yonadabu alimusukuma Amunoni kusema uwongo; kumukosea Tamari; kuasi sheria ya Mungu. Mungu anakataza ushirika wa ndoa na binti aliyezaliwa na baba yako. Angalia Walawi 18:11).

Unapashwa kufanya nini wakati marafiki wanakuomba kutenda mabaya? (Usiwasikilize, kataa kushiriki). Fanya angalisho usiwe sawa Yonadabu. Usiwasukume hata kidogo marafiki wako kutenda zambi!

2. Ukali wa Abusaloma (2 Samweli 13:18-39.)

Tamari alikuwa na kaka yake mwengine aliyeitwa Abusaloma. Aliona Tamari akilia kwa huzuni. Akauliza: "Amunoni alikukamata kwa nguvu kulala naye?

Tamari akatikisa kichwa kwa kuitika. Palepale Abusaloma akamuchukia Amunoni. Akafikiri, nitalipiza kisasi. Baba hakumwazibu. Lakini hataponyoka kosa alilotendea dada yangu.

Miaka miwili ikapita. Halafu siku moja Abusaloma akamwendea mufalme Daudi. Akasema: "Ni wakati wa kukata manyoya ya kondoo. Ninatayarisha kufanya karamu kubwa. Je, unaweza kuja wewe pamoja na wana wako wote?"

Daudi akajibu: "Hapana, mwana wangu. Tukikuja sisi wote itakuwa garama kubwa kwako." Abusaloma akasihi: "Kama wewe baba hautakuja, utume Amunoni kwa nafasi yako." Mufalme Daudi akakubali. Halafu wana wake wote walihuzuria kwenye karamu.

Wakati ule Abusaloma alikuwa amekwisha kufanya shauri mbaya juu ya Amunoni. Akaita watumishi wake wamoja kuja kwake. Akawanongoneza: "Nitakapowafanyia kitambulisho, mumwue Amunoni."

Halafu karamu ya Abusaloma ikageuka kuwa kitisho.

Onyesha taswira 10: Amunoni aliuawa. Ndugu zake wengine wote wakakimbia juu ya nyumba zao. Kwa kuokoa uzima wake yeye mwenyewe, Abusaloma alifichama katika inchi ya Gesuri.

Daudi, mufalme alivunjika moyo aliposikia yale yaliyotendeka. Maneno ya Natana yalianza kutendeka kwa kweli: "Zambi yako itakuletea huzuni na kwa jamaa lako." Tendo la uovu la Abusaloma lilimukumbusha Daudi kuhusika kwake na kifo cha Uria. Je, angeweza kufanya kosa kwa kumwazibu mwana wake sababu ya uuaji? Angeweza. Baba anahitaji kufundisha mwana wake kutenda haki.

3. Uasi wa Abusaloma (2 Samweli 14:1 hadi 18:33.)

Miaka tatu ikapita. Abusaloma alibaki Gesuri. Aliogopa kurudia katika nyumba ya kifalme. Alijua kama alistahili kifo kwa yale aliyotenda.

Siku moja, Yoabu Jemadari wa mufalme Daudi, akamupelekea Abusaloma ujumbe. Alisema: “Abusaloma, baba yako anakukumbuka. Anataka urudie Yerusalema.”

Abusaloma akasema kwa sauti: “Vema! Basi amenihurumia.,” Yaobu akasema: “Vizuri, hakukusamehe kabisa. Anasema hautaishi katika nyumba ya kifalme. Na hautaweza kumwona.” Kwa hiyo Abusaloma akarudia Yerusalema. Lakini hakuweza kumwona baba yake. Wala hakuweza kuishi pamoja naye.

Miaka mbili ikapita. Mufalme Daudi kwa mwisho akaalika Abusaloma kuishi katika nyumba ya kifalme.

Tangia pale, Abusaloma alijaribu kugeuza watu wamwasi mufalme. Fikiri juu ya yale! Abusaloma alikuwa na sura nzuri - kijana mwenye sura nzuri sana kuliko vijana wote wa Israeli. Alikuwa na nywele ndefu na nzuri sana ambazo alijivunia sana. Kwa uzuri wake, Abusaloma alivuta mioyo ya wanaume na wanawake. Zaidi ya vitu vingine vyote, Abusaloma alitaka kuwa mufalme. Je, hii ilikuwa tamaa nzuri kwake? (Hapana. Mungu alimuchagua Daudi kuwa mufalme.)

Onyesha taswira 11: Siku kwa siku Abusaloma alikaa kwenye milango ya muji. Wakati watu walipokuja kumwona mufalme Daudi, Abusaloma aliwasimamisha. Aliuliza: “Munatoka wapi? Matata yenu ni gani?”

Alisikiliza magumu yao. Halafu alisema: “Baba yangu iko na kazi nyingi sana hata aweze kuwasaidia. Ningelikuwa mufalme, ningeliweza kuwasaidia. Ningeliwatendea kwa usawa. Ningeliwapa haki zenu. Lakini siko mufalme. Angalia ginsi ninatamani kuweza kuwasaidia!”

Halafu Abusaloma aliweza kushika mikono yao na kuwabusu. Watu wakavutwa na huyu mwana wa mufalme anayekuwa na sura nzuri. Nyuma kidogo walikuwa wakisema: “Labda tungemufanya Abusaloma kuwa mufalme.”

Hii ndiyo Abusaloma alitaka kabisa kusikia. Halafu, alikuwa na uhakika kwamba watu wa kutosha walichagua upande wake. Kwa hiyo akafanya mipango ya kupindua mufalme Daudi. Fikiri juu ya hayo! Abusaloma anafanya shauri mbaya la kumwua baba yake mwenyewe na kuchukua kiti cha kifalme. Unafikiri alizungumuza na Mungu juu ya mipango yake? (Hapana. Hakuna aya inayosema kama Abusaloma aliendelea kuomba Mungu.)

Halafu Daudi akapata habari kuhusu yale Abusaloma alipanga kufanya. Kwa kweli mufalme Daudi alikumbuka maneno ya nabii. “zambi yako italeta hasara kwako na kwa jamaa lako.” Maneno ya nabii Natana yalikuwa ya kweli.

Mufalme pamoja na wafuasi wake wakakimbia toka Yerusalema. Abusaloma na watu wake wakakamata muji. Kisha kidogo, vita vya kindani vikaanza. Baba na mutoto walipigana kati yao. Moyo wa Daudi ulivunjika. Hakupenda vita kama hii. Akalia. Na wale waliomupenda wakalia pamoja naye. Sasa Daudi akasema na rafiki yake wa kweli. Huyu alikuwa nani? (Mungu). Daudi alimupenda Mungu na Mungu alimupenda Daudi, mufalme. Mungu alisikia maombi ya Daudi? Sikiliza!

Abusaloma aliendea watu wawili kati ya watu wake kwa kuomba shauri. Kila mumoja alimupatia mawazo tofauti kwa kumushambulia mufalme Daudi. Abusaloma alijiuliza ni shauri la mutu gani ndilo lililokuwa bora. Kwa mwisho akakata shauri. Halafu akaanzisha mashambulio yake juu ya Daudi na watu wake. Lakini alishindwa katika vita na kupoteza uzima wake (2 Samweli 18:14-15) Bwana alimusukuma Abusaloma kufuata shauri mbaya. Kila mara Mungu anatawala. Yeye anayekuwa Bwana juu ya yote anatawala mioyo, mafikiri, na makusudio.

4. Toba ya Daudi (2 Samweli 19:1-8.)

ABUSALOMA ANAKUFA! ABUSALOMA ANAKUFA! Unafikiri Daudi alijisikia namna gani aliposiki habari hii? (Sukuma wanafunzi wazungumuze). Ijapokuwa Abusaloma aliasi baba yake, Daudi aliendelea kumupenda. Mufalme hakupenda yale Abusaloma aliyofanya. Lakini Abusaloma alikuwa mwana wake.

Onyesha taswira 12: Akiwa na moyo wenye kuvunjika, mufalme Daudi alienda katika chumba chake peke yake. Akalia: “Ee mwana wangu Abusaloma, mwana wangu, mwana wangu Abusaloma! Ikiwa tu ningeweza kufa kwa pahali pako!” Daudi alikuwa akivuna matokeo ya zambi zake. Tena Mungu alifazaisha jamaa la Daudi.

Nyuma ya kifo cha Abusaloma, mufalme Daudi akarudia Yerusalema kwa kutawala. Wale waliomupinga, wakawa tena waaminifu kwake.

Mafundisho gani mumepata toka matukio haya katika maisha ya Daudi?

1. Kama vile watoto wa Mungu, tunapashwa kuogopa zambi. Mungu hafungi macho yake juu ya zambi. Kama vile baba mwenye upendo, Yeye anaazibu zambi.
2. Usisikilize marafiki wanaokushawishi kutenda mabaya.
3. Usiwashawishi wengine kutenda zambi.
4. Uwe hakika kama tamaa zako zinamupendeza Mungu.
5. Yale unayopanda ndiyo utakayovuna. (Wagalatia 6:7)
6. Unazuru wengine wakati unafanya zambi.

Namna gani tunaweza kujilinda na maisha ya zambi?

1. Kujifunza Neno la Mungu na kulishika
2. Kuomba kwa ajili ya kila kitu
3. Acha Roho Mutakatifu akuongoze kila siku.
4. Zungumuza juu ya kazi na mipango yako pamoja na viongozi Wakristo wanaopenda Biblia.

SOMO 4 - MUFALME DAUDI NI MWEPESI KUSIKILIZA MUNGU.

Kwa mwalimu kujifunza mbele: 2 Samweli 21 hadi 24

Shabaa ya somo: Kuonyesha kama Mungu , Mufalme juu ya vyote ni mwenye huruma na mwema.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kwamba Mungu anataka watumishi wake wamuheshimu na kumutii.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Heshima kubwa kwa ajili ya Mungu wetu mukubwa.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kusifu Mungu kwa ajili ya upendo na rehema yake.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Mufalme Daudi anahesabu Waisraeli (2 Samweli 14:1-9; 1 Mambo ya siku 21:1-7)
2. Mufalme Daudi anatubu na kuabudu (2 Samweli 24:1-25; 1 Mambo ya siku 21:8-30)
3. Mufalme Daudi anatii mapenzi ya Mungu (1 Mambo ya siku 22:1-19; 28:1-21)
4. Mufalme Daudi anamutukuza Mungu (2 Samweli 22:1-51)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Tumainia Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe: katika njia zako zote umukiri yeye, naye ataongoza mapito yako.
Mezali 3:5-6

Maelezo kwa mwalimu:

Kwa kufunga mufululizo huu, rudilia maarifa makubwa ya maisha ya Daudi. Tia mukazo juu ya ushuhuda wa Mungu juu ya Daudi - "Mutu anayependeza moyo wa Mungu." Hii haina maana kusema kama daudi alikuwa mukamilifu. Lakini alimupenda Bwana kwa kweli na alitaka kumupendeza. Ingawa vile, kwa mara nyingi alikosa kumwamini Mungu. Kila mara alikiri zambi zake kwa Bwana na kuomba musamaha. Bwana alijua kama kwa kweli Daudi alitaka kufanya mapenzi ya Mungu (Matendo 13:22), hivi alikuwa "mutu mwenye kupendeza moyo wa Mungu." (1 Samweli 13:14; angalia 16:7)

Maisha ya daudi ni ya kututia moyo. Tunapofanya kosa, tunapashwa kukiri zambi yetu kwa Mungu. Halafu kama tuko wazi kwa kweli, Atatuhurumia. Lakini tunapashwa kwa bidii uwezekano wote tusifanye kosa tena.

Unaweza kufasiria maana ya "uwanja wa kupepete." Ni nafasi ambako mbegu zinatengwa na maganda ao majani makavu kwa kupigapiga.

Somo: Leo hii hapa, kuna mutu yeyote anayekuwa mukamilifu?… Yule ambaye hajatenda HATA KIDOGO mabaya? (Hapana!). Ni mutu moja tu aliweza kuishi katika dunia ndiye aliyekuwa mukamilifu. Alikuwa nani? (Bwana Yesu Kristo).

Namna gani Mungu anatoa maelezo juu ya Daudi? (Mutu anayependeza moyo wa Mungu). Hii ina maana kama yuko mukamilifu? (Hapana). Namna gani tunajua kama alikuwa mukamilifu? (Mungu ameandika katika Neno lake zambi za Daudi.) Bwana aliendelea kumupenda Daudi? Daudi aliendelea kumupenda Mungu? Kila wakati Daudi alipokiri kwa kweli zambi zake, Mungu alimusamehe. Kwa kweli Daudi alitaka kuheshimu Bwana na kumupendeza. Kwa sababu ya hii aliendelea kuwa "mutu anayependeza moyo wa Mungu"

1. Mufalme Daudi anahesabu Waisraeli (2 Samweli 24:1-9; 1 Mambo ya siku 21:1-7.)

Abusaloma alipokwisha kufa, mufalme Daudi akarudia Yerusalema. Tena alikaa juu ya kiti cha kifalme. Mara tena amani ikawekwa katika inchi ya Israeli. Ingelikuwa vizuri sana kusema: "Halafu kila mara Daudi alimupendeza Mungu." Lakini hii haingelikuwa kweli.

Siku moja Daudi akaita Jemadari Yoabu kwenye nyumba ya kifalme. Mufalme akaamuru: “Ufanye hesabu ya watu wote wa Israeli. Ujue ni wanaume ngapi wanaweza kwenda kwa vita.”

Jemadari Yoabu akauliza: “Kwa nini unataka kufanya vile? Waisraeli wote ni watu wako. Kwa nini unahitaji kujua wako ngapi? Unajivunia nguvu yako?

Mufalme akaamuru: “Fanya vile ninavyosema!”

Onyesha taswira 13: Jemadari Yoabu pamoja na wakubwa wa waaskari wakatii. Kwa karibu muda wa miezi kumi walikwenda katika kila muji wa Israeli. Mumoja kwa mumoja, kila mutu aliandikwa. Kwa mwisho watu wote wakahesabiwa.

Bwana hakumwambia Daudi afanye vile. Daudi hakumwuliza Mungu kama mupango huu unamupendeza. Bwana alichunguza ndani ya moyo wa Daudi. Akaona kwamba Daudi hakuaminia uwezo wa Mungu. Aliaminia ukubwa wa jeshi lake. Bwana Mungu hakupendezwa.

2. Mufalme Daudi anatubu na kuabudu (2 Samweli 24:1-25; 1 Mambo ya siku 21:8-30.)

Nyuma ya miezi, Jemadari Yoabu akaleta habari yake kwa mufalme. Kwa gafula Daudi akatambua kwamba alifanya zambi. Akauliza Bwana: “Kwa nini ninafanya hivi? Nilijivuna. Nilikuwa nikitegemea nguvu ya jeshi langu. Sikukuaminia Wewe, Mungu. Tafazali unisamehe. Nimetenda kwa jinga kabisa.”

Bwana alimusamehe Daudi. Lakini tena matokeo ya zambi yake yalizuru wengine.

Mungu alituma nabii aliyeitwa Gadi na ujumbe. “Mufalme Daudi, Mungu atakuadibisha kwa ajili ya zambi zako.” Gadi aliendelea kusema: “Kwa mara hii utachagua azabu yako: (1) Utapata miaka saba ya njaa katika inchi. Ao (2) Utakimbia adui zako muda wa miezi tatu. Ao, (3) Mungu atatuma siku tatu ya tauni katika inchi. [Fasiria kama tauni ni ugonjwa wa kuangamiza unaoambukia.] Ufikiri juu ya ile na uchague moja.”

Uamuzi muzito wa namna gani gani huu Daudi alipashwa kufanya! Kwa mwisho Daudi akakata shauri. Akaenda kwa nabii Gadi. Akasema: “Acha tuanguke katika mukono wa Bwana. Rehema yake ni kubwa. Usiniacha kuanguka katika mukono wa mutu. Ninachagua siku tatu ya tauni katika inchi.”

Halafu Bwana akatuma tauni. Siku moja, siku mbili, siku tatu, watu walikufa. Daudi alivunjima moyo. Akalia: Ee Mungu, mimi ndiye nilifanya zambi. Mimi ndiye nilikosa. Watu hawa hawakufanya kosa. Tafazali uniazibu mimi na jamaa langu. Lakini rehemu watu wangu.”

Mungu akatuma ujumbe mwingine kwa mufalme Daudi kupitia nabii wake. “Kwenda ujenge mazabahu juu ya uwanja wa kupepetea ngano wa mutu anayeitwa Arauna.” Mufalme Daudi alijua yale yaliyotendeka pale miaka mingi mbele. Pale ilikuwa nafasi Abrahamu alitoa mwana wake Isaka. (Kwa kifupi urudilie tukio toka Mwanzo 22). Palepale mufalme Daudi akatii Bwana.

Arauna aliona mufalme Daudi na watumishi wake wakikaribia. Kwa woga, Arauna akainama mbele ya mufalme. Akauliza: “Kwa nini bwana wangu mufalme anakuja kwangu?”

Daudi akafasiria: “Ninataka kununua kiwanja chako cha kupepetea ngano. Juu yake nitajenga mazabahu kwa ajili ya Bwana Mungu. Halafu atazuia tauni katika inchi yetu.”

Arauna akasisitiza: “Ee mufalme, nitakupatia kiwanja kile. Unaweza kutwaa ngombe dume wangu kwa ajili ya sadaka. Twaa vifaa vya kupepeta. Tumia nira kwa ajili ya moto wa kuteketeza sadaka. Vyote ni vyako. Hauhitaji kulipa kitu chochote.

Onyesha taswira 14: Sikiliza jibu la mufalme: “Hapana, Arauna. Sitakamata vitu hivi vyote kama zawadi. Nitavinunua. Sitatolea Bwana Mungu sadaka za kuteketezwa zisizokuwa na bei kwangu.”

Daudi akalipa kila kitu na kutolea sadaka ambazo Mungu aliamuru. Mungu aliangalia ndani ya moyo wa Daudi. Aliona kaka mufalme alihuzunika kwa kweli kwa ajili ya zambi zake. Bwana akapendezwa. Alisamehe Daudi na kuzuia tauni. Lakini watu 70.000 walilala maiti.

3. Mufalme Daudi anatii mapenzi ya Mungu (1 Mambo ya siku 22:1-19; 28:1-21.)

Wakati ulifika Daudi alipotaka kujengea Mungu hekalu nzuri. Lakini Bwana akasema: “Hapana,Daudi. Umepigana vita mara nyingi na kumwanga damu nyingi. Hautajenga hekalu langu. Tafazali mwana wako Solomono atajenga nyumba kwa ajili ya jina langu.” (1 Mambo ya siku 22:8-10).

Onyesha taswira 15: Daudi angeliweza kukasirika sababu Mungu alikataa maombi yake. Kuliko vile, alichapa taswira kwa ajili ya ujenzi wa Hekalu. Alikusanya vifaa ambavyo Solomono alihitaji kwa ajili ya jengo. Aliamuru viongozi wa Israeli wamusaidie Solomono. Alichagua watu wenye akili kwa kufanya kazi. (Angalia 1 Mambo ya siku 22).

Unafikiri ni wapi Hekalu la Mungu lilipashwa kujengwa? Ni kwa nafasi ile ile Daudi aliyonunua toka kwa Arauna. Kwa hiyo Daudi alikuwa amenunua nafasi ya Hekalu. Alinunua na mali yake mwenyewe. Lakini hakuruhusiwa kujenga Hekalu la Mungu.

Daudi hakukasirika sababu hangeweza kufuata njia yake mwenyewe. Hakupata wivu sababu ya Solomono. Alimutii Mungu kabisa kabisa. Mufalme alifurahi kwa ajili ya upendeleo ambao Solomono atakaopata. Sikiliza shauri la mufalme Daudi kwa mwana wake Solomono. (Soma polepole 1 Mambo ya siku 28:9). Hilo ni shauri nzuri kwa ajili ya kila mumoja wetu.

4. Mufalme Daudi anasifu Mungu (2 Samweli 22:1-51.)

Alipokuwa angali anaishi, Daudi aliandika nyimbo kwa ajili ya Mungu. Kitabu cha Biblia cha Zaburi kinakuwa na nyimbo hizo nyingi ndani yake. Zingine nyimbo mbili za Daudi zinaonekana kwa mwisho wa kitabu cha pili ha Samweli. Mara na mara daudi aliimba nyimbo hizi kwa zeze yake.

Onyesha taswira 16: Katika wimbo moja, Daudi aliita Mungu ni mwamba, boma lake la nguvu na kimbilio lake (2 Samweli 22:2-3). Alitaka kusema nini? (Bwana ana nguvu; wale wanaomwamini wako salama).

Anasema juu ya Mungu kama ni yule anayeokoa toka jeuri (2 Samweli 22:3). Anaponyesha toka katika hatari (2 Samweli 22:18). Haya yanatuambia nini? (Mungu ana nguvu sana, analinda na kukinga).

Mungu alimupa Daudi zawadi alipokuwa mutiifu. (Angalia 2 Samweli 22:21, 25). (Mungi ni Mwema).

Mungu alimwongoza Daudi. (2 Samweli 22:29). Mungu anatupatia akili vilevile. (Angalia Yakobo 1:5)

Kwa kweli Daudi alitaka kufanya mapenzi ya Mungu. lakini mara na mara alifanya makosa. Wakati wowote alipofanya makosa, alihuzunika kwa kweli na kutubu. Aliomba musamaha kwa Mungu. Aliomba kwamba Mungu aweze kumupatia misimamo mizuri katika kila jambo. Juu ya vingine vyote, Daudi alitaka Bwana Mungu apate kuheshimiwa.

Daudi alikuwa mufalme wa Mungu. Bwana alimuchagua kwa kutawala juu ya kiti cha kifalme cha Israeli. Mungu alimupatia ushindi juu ya maadui wake. Bwana Mungu alimwazibu Daudi wakati alifanya zambi. Mungu alimukinga Daudi wakati wengine walitaka kumuangamiza. Bwana alitumia Daudi kwa kutimiza makusudi yake.

Nyuma ya miaka mingi, muda murefu kisha kufa kwa Daudi, Mungu akamuheshimisha kwa namna ya kushangaza. Bwana Yesu akazaliwa toka kwa mumoja wa wazao wa Daudi. (Angalia taswira 16 upande wa juu). Agano Jipya inasema juu ya Kristo kama “Mwana wa Daudi” (Matayo 1:6; 9:27; 22:42).

Leo Bwana Mungu ni Mufalme wetu. Ni Mutawala wa ulimwengu wote. Aliweka wewe na mimi kwa nafasi hii. Anataka sisi - kama alivyotaka Daudi - tumutii Yeye. Yuko na mupango kwa ajili yako na kwa ajili yangu. Zaidi ya mengine yote, anataka tumusifu yeye na kumuheshimu.

Mungu anataka kila Mukristo awe mutu “anayependeza moyo wa Mungu.” Namna gani tunaweza kufanya vile? (Kwa kutii wale wanaokuwa na mamlaka juu yetu. Kwa kuwaelezea wengine kwamba Bwana Yesu alikufa kwa ajili yao. Kwa kuimba nyimbo zinazomutukuza Bwana. Kwa kusema “Hapana” wakati tunajaribiwa kufanya makosa.)

Namna gani mutu asiyeamini anaweza kuwa mutu anayependeza moyo wa Mungu? (Uamini Kristo na kumupokea kama vile Mwokozi wako wa kipekee). Halafu atakupatia moyo unaotaka kupendeza Mungu. Hauwezi kumupendeza kwa nguvu yako mwenyewe. Hautakuwa mukamilifu. Lakini utataka kumupendeza Bwana. Na kama unamutegemea, atakusaidia kila mara.